

JINA: ..... ADM NO .....

SHULE: .....

TAREHE: .....

MUDA: MASAA 2 NA NUSU

# kiswahili karatasi ya 1

---

## KIDATO CHA TATU MUHULA WA TATU

ATIKA SCHOOL

ALL SEASONS

### MAAGIZO

- 1) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- 2) Jibu maswali yote.
- 3) Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali

# 1. UFAHAMU

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:*

Zamani wanadamu wa kwanza ambao ni mababu wa vizazi vingi vilivyopita waliishi duniani. Habari kuhusu maisha na maumbile yao haikujulikana kwa hakika kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kuandika. Lakini mara kwa mara shughuli za Wanaakiolojia kama Louis Leakey na wengine hugundua mifupa yao ardhini na michoro yao katika mapango. Wataalamu hawa hufukua mafuvu, vyombo na silaha zao za zamani. Kwa kuchunguza vitu hivi tunaweza kubahatisha viumbe hawa walivyokuwa na jinsi walivyoishi. Moja ya mambo yanayofahamika sasa ni kuwa wanadamu hawa wa awali walifanana na sokwe. Aidha, walitembea kwa kupinda mgongo kama kibiongo. Chakula na uhai wao ulitegemea kukusanya matunda, kokwe, majani ya miti na mayai ya ndege. Vilevile, walitegemea wanyama wadogo, kufukua mizizi na kubambua magamba ya miti walipokabwa na njaa.

Maisha yao yalikuwa ya hatari. Walikuwa wakiwindwa na wanyama wakubwa. Hii ni kwa sababu mwanzoni hawakuwa na silaha za kujihami. Hivyo iliwabidi kujificha katika miti na vilima kuepuka uvamizi. Lakini usalama wao ulitegemea kwa kiasi kikubwa kudura za Mungu au pengine miungu. Kwa taratibu wanadamu hawa walijifunza kutengeneza silaha. Walianza kwa kutumia fimbo nene zenye ncha au mawe ya kutupia. Baadaye walichonga mawe ili kuyafanya kuwa visu, nyundo au vigumba vya mikuki. Hatimaye, walivigomoa au kupasua vipande vya mawe na kuvitumia kama mishale. Hapa ndipo walipoanza kuwinda wanyama wakubwa, mithili ya swara, nguruwe, nyati na ngiri, pia waliweza kutumia mikuki kudunga samaki majini.

Mababu zetu hawakuwa na nyumba. Kwanza walikuwa wakijisitiri kwa kukaa chini ya vivuli vya miti au kujenga vibanda vya matawi na majani ya miti. Hawakuweza kuingia mapangoni asilani kwa kuchelea wanyamapori wakali kama chatu, simba na mamba waliokaa humo. Kwa bahati, siku moja mmoja wao aligundua moto alipokuwa akipekecha vijiti. Kabla ya ugunduzi huu, wao pia hawakujua kazi ya moto na walikuwa wakiogopa na kukimbia moto jinsi wafanyavyo wanyama wa mbungani mpaka wa leo. Ujuzi wao wa kutumia moto ulileta mabadiliko makubwa. Baada ya hapo waliweza kukaa mapangoni na kukoka mioto milangoni mwa mapango ili kuwaogofya adui. Halikadhalika, waliweza kuota moto, kumulika maskani yao mapya na kuchoma nyama badala ya kuila mbichi.

Wanadamu wa awali hawakuwa na mavazi. Waliwezaje kuzuia baridi? Inadhaniwa kwamba nywele nyingi walizokuwa nazo kwenye mwili zilisaidia kuwapa joto. Uvaaji wa nguo ulianza walipoanza kutumia ngozi kutoka kwa wanyama waliowawinda. Walizisafisha ngozi kwa kuzipaa kwa kombe za mawe na kuzianika juani. Zilipokauka walizivaa kwa kujifunga na kuzishikanisha kwa mifupa au mikanda ya ngozi. Wanadamu hawa hawakuweza hata kuongea. Waliwasiliana kwa kupiga mayowe, kutoa milio au kunguruma jinsi wafanyavyo wanyama. Polepole walianza kutumia sauti na baada ya muda walizipanga sauti kuibua mfumo wa maneno yenye maana za kipekee. Umilisi wa kutumia lugha uliwawezesha kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Lugha pamoja na matumizi ya moto na silaha viliwarahisishia maisha na kuwawezesha kupata muda wa kupumzika mapangoni jioni wakiota moto. Kutokana na hali hii waliweza kutekeleza jambo moja kuu waliloturithisha. Walitupokeza sanaa. Kutoka kwao tulirithi fasihi simulizi na kupata nakshi za michoro yao kwenye mapango. Michoro hii inapatikana katika mapango hata leo hii nchini Ufaransa, Uhispania, Afrika Kusini na hata Afrika Mashariki.

(a) Msemu, “kudura za Mungu au pengine miungu” inadhihirisha hali gani ya wanadamu wa kwanza. (alama 2)

---

---

(b) Kwa nini wanadamu hawakuishi mapangoni mwanzoni? (alama 2)

---

---

(c) Fafanua mambo **matatu** yaliyomwezesha mwanadamu wa kwanza kupiga hatua kimaendeleo. (alama 6)

---

---

---

---

---

---

---

---

(d) Taja sifa **mbili** za Kimaumbile zilizowatofautisha wanadamu wa awali na siku hizi. (alama 2)

---

---

(e) Eleza maana ya:- (alama 3)

(i) Walipokabwa: \_\_\_\_\_

(ii) Kujihami: \_\_\_\_\_

(iii) Maskani: \_\_\_\_\_

## 2. UFUPISHO

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia*

Lugha imekuwa kikwazo kikubwa katika kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) barani Afrika. Lugha ambazo zimekuwa zikitumiwa ni za kimagharibi kama vile Kijerumani, Kifaransa na Kiingereza. Idadi kubwa ya Waafrika, hawa wanaoishi vijijini, hawazifahamu lugha hizi. Uamuzi wa Shirika la Microsoft wa kutumia lugha ya Kiswahili katika programu za kompyuta kuanzia mwaka 2005 ni mchango mkubwa. Kuzinduliwa kwa mradi huu ni tukio la kipekee kuimarisha teknolojia sehemu za mashambani. Mradi huu umewawezesha wananchi takribani milioni 150 wa janibu za Afrika Mashariki kufaidi huduma za tarakilishi.

Utekelezaji wa mradi huu halikuwa jambo jepesi. Kwanza, ilibidi Shirika la Microsoft chini ya uongozi wa Bill Gates kuliwasilisha Bodi lake la Wakurugenzi. Bodi liliposhawishika kuwa Kiswahili ni lugha inayotumiwa na mamilioni ya watu liliidhinisha kuzinduliwa kwa mradi. Hatua iliyofuatia ilikuwa kuteua maneno 700,000 ya kimsingi ya Kiingereza ambayo yangetafsiriwa kwa Kiswahili. Hatua iliyofuata ilikuwa ya kutafuta ushirikiano na dola pamoja na mashirika ya kibiashara na taasisi za kielimu ulimwenguni. Ilipobainika kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yangehamasisha uwekezaji katika vituo vya mtandao vijijini, ushirikiano katika kuendesha mradi huu uliafikiwa bila shida. Mradi huu ulichukua muda wa miezi 18 kukamilika. Uliwashirikisha wahusika katika uwanja wa teknolojia ya habari, mawasiliano, elimu, biashara na idara za Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Vyuo vikuu hivi ni pamoja na Dar es Salaam, Nairobi, Kenyatta na Makerere.

Wataalamu walioshirikishwa walisaidia katika kubuni faharasa ya istilahi za Kiswahili 3,000. Hizi ni zile ambazo zinafaa kwa matumizi ya kompyuta ya kawaida na ya kila siku. Mradi huu umeshangiliwa na wekereketwa na wapenzi wa Kiswahili katika Nyanja zote. Wasomi, wanariadha, wanamuziki, watalii, wafanyabiashara, wanasiasa, wafuasi wa dini mbalimbali na wakulima; wote wamefurahia hatua ya Kiswahili kuingizwa kwenye mtandao. Watu ambao walikuwa hawawezi kutumia tarakilishi kwa sababu ya kutojua Kiingereza sasa hawana kisingizio. Matumizi ya Kiswahili yatapanua na kuimarisha mawasiliano baina ya watu wanaoishi vijijini na pembe zote za ulimwenguni. Jambo la kutia moyo zaidi ni kuwa sasa vyuo vikuu vinavyotoa masomo kwa kutumia mitandao vimepewa idhini ya kutumia programu hizi. Walimu na wanafunzi wanapata habari moja kwa moja kwa Kiswahili bila kutafsiri. Kuna uwezekano sasa wa kusambaza mafunzo katika Nyanja na viwango vyote kwa mfumo wa elimu ya mbali. Katika ulimwengu wa utandawazi, tukio kama hili lina manufaa makubwa. Wananchi wa vijijini wanaweza kupata habari na maarifa kutoka pembe zote za dunia na kuhusu maswala tofauti kwa lugha wanayoielewa barabara.

Kusambaa kwa matumizi ya ngamizi vijijini kutaimarisha biashara inafungamana na teknolojia ya mawasiliano. Hali hii itainua maendeleo ya kiteknolojia na kiwango cha maisha vijijini. Bila shaka mwachano uliopo baina ya sehemu za mijini na vijijini utapungua. Haya ndiyo maendeleo anayokamia kila mja wa siku hizi. Lililopo ni serikali kupania kupanua na kusambaza muundo mbinu kama umeme na simu katika sehemu zote za nchi. Pamoja na haya, kuna haja ya kupunguza bei ya ngamizi na vipuri vyake ili kuwatia motisha watu kununua kompyuta kwa wingi. Ikumbukwe kuwa lengo la kuanzisha mradi huu lilikuwa kuisaidia serikali kupanua na kusambaza matumizi ya huduma za kompyuta na mtandao katika shule, vituo vya kijamii na maeneo ya makaazi. Huduma hizi ni msingi wa elimu, biashara na mawasiliano ya kisasa.





### 3. MATUMIZI YA LUGHA: ALAMA 40

- (a) Eleza tofauti kati ya sauti p / na / b / (alama 2)

---

---

- (b) Bainisha **kivumishi** na **kielezi** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)  
Juma alinunua gari lake kwa kulipa pole pole.

---

---

- (c) Geuza maneno yafuatavyo katika kauli ya **kutendesha**. (alama 2)

(i) Ogopa: \_\_\_\_\_

(ii) Nawa: \_\_\_\_\_

- (d) Ziweke nomino zifuatazo katika **ngeli** zake. (alama 3)

(i) Saa: \_\_\_\_\_

(ii) Chai: \_\_\_\_\_

(iii) Uchoyo: \_\_\_\_\_

- (e) **Yakinisha** sentensi hii. (alama 2)  
Asingekuwa anampenda asingemnunulia zawadi.

---

---

- (f) Tumia '**O**' **rejeshi** kuunganisha sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Gurudumu hili ni zuri.

(ii) Gurudumu hili litanunuliwa.

---

---

- (g) Andika katika **msemo** wa taarifa. (alama 3)  
“Ah! Mto huu ni mpana. Je, utaweza kuuvuka?” Naomi aliuliza.

---

---

- (h) Tunga sentensi **mbili** ukitumia viunganishi vifuatavyo; (alama 2)

(i) Seuze: \_\_\_\_\_

---

(ii) Ila: \_\_\_\_\_

---

- (i) Andika sentensi ifuatayo katika **wingi** hali ya **ukubwa**. (alama 2)  
Kigoma chako chapendeza:

---

---

- (j) Tunga sentensi **kubaini nomino** ya kitenzi jina. (alama 2)

---

---

- (k) Andika **wingi** wa sentensi hii. (alama 2)  
Ukiziba ufa utajenga ukuta.

---

---

- (l) Ainisha **fungutenzi** ifuatayo. Unatembea. (alama 2)

---

---

- (m) Changanua sentensi ifuatayo kwa **njia** ya **mstari**. (alama 4)  
Mwanafunzi mwerevu anaishi Nairobi.

---

---

---

(n) Onyesha shadda la neno hili. Matukio. (alama 1)

---

(o) Andika **kinyume** cha maneno **yaliyopigiwa mstari**. (alama 2)  
Mama aliinjika chungu mekoni mvua iliponyesha.

---

---

(p) Toa maana **mbili** ya sentensi hii. (alama 2)  
Mfinyanzi hulia gaeni.

---

---

(q) Kamilisha jedwali hili. (alama 4)

Nomino	-pi	-chache	-ingi	gani
Manukato				
Uchaguzi				

(r) Tunga sentensi moja kwa kutumia kiwakilishi cha 'a' unganifu.

(alama 1)

---

---

## SEHEMU YA E: ISIMU JAMII: (ALAMA 10)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

“Semeni Amen. Ndugu atamsaliti mtoto na mtoto atamsaliti mzazi. Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu kwa ajili ya jina langu, lakini mwenye kusubiri hadi mwisho ataokoka”

(a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. (alama 2)

---

---

---

---

(b) Fafanua sifa za sajili iliyotumiwa katika mazungumzo haya. (alama 8)

---

---

---

---

---

---

---

---